

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Ludewa Agosti 15, 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Sensa ya Watu na Makazi Wilaya ya Ludewa ambaye pia na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere leo Agosti 15, 2022 amewataka wasimamizi wa Mahudhuhi, wasimamizi wa TEHAMA na Makarani wa Sensa wilayani humo wanao endelea na mafunzo kuwa makini katika matumizi ya vifaa vya Sensa vikiwemo **VISHIKWAMBI**.

Ameyasema hayo alipokuwa akitazama mwenendo wa mafunzo yanayo endelea katika vituo vinne vya mafunzo wilayani Ludewa na akaongeza kwa kusema kuwa, watakao zembea na kupoteza vifaa hivyo watachukuliwa hatua.

Aidha amewaomba wananchi wote wa Wilaya ya Ludewa ifikapo tarehe 23/08/2022 kila mwananchi wa Wilaya ya Ludewa ahakikishe anahesabiwa.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa**



*Jiandae kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*